



HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA

Taarifa Namba: 025

25 Julai 2021

Barua pepe: td@tundumatc.go.tz Tovuti: www.tundumatc.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

TUNDUMA YAKUSANYA MAPATO KWA ASILIMIA 118 YAVUKA LENGU LA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Halmashauri ya Mji Tunduma imevuka lengo la kukusanya Mapato yake ya ndani kwa kufikisha makusanyo ya shilingi **Bilioni 6.3** ikiwa ni **asilimia 118%** ya lengo la mwaka wa Fedha wa 2020/2021 uliofikia ukomo mwezi uliopita yaani tarehe 30 Juni 2021.

Katika mwaka wa Fedha wa 2020/2021 ulioanza Julai Mosi mwaka 2020 Halmashauri iliweka lengo la kukusanya Shilingi **Bilioni 5.3** kupitia vyanzo vyake vya ndani. Makusanyo haya yenye tija katika kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ustawi wa watu wa Tunduma, yamepatikana kupitia vyanzo mbalimbali vikiongozwa na vyanzo vikuu ambavyo ni **Tozo ya Mazao mbalimbali, Tozo za usafi wa mazingira, Tozo ya Lesseni za Biashara, ushuru wa huduma, na Ushuru wa Malazi**

Baada ya kufikiwa kwa mafanikio haya Uongozi wa Halmashauri Tunatoa shukrani za dhati kwa **Makampuni, Wafanya Biashara wakubwa, Wafanya Biashara wadogo, Taasisi za Umma, Taasisi Binafsi** pamoja na **wananchi kwa ujumla** kwa ushirikiano mkubwa wa kulipa tozo halali za kiserikali zilizowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi kwa kipindi chote cha mwaka wa fedha 2020/2021

MWISHO: Uongozi unawakumbusha kuwa **mwaka mpya wa fedha wa 2021/2022 umeanza rasmi** tangu tarehe Mosi mwezi huu hivyo tunatarajia ushirikiano mkubwa katika ulipaji wa tozo za Halmashauri kupitia bajeti mpya yenye makadirio ya Zaidi ya shilingi **Bilioni 5.6**

Imetolewa na;

William K. Maganga

William K. Maganga
**AFISA HABARI NA MAWASILIANO
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**